

Tangazo hili limeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA).

(Imesajiliwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 [Toleo la Mwaka 2002])
(cheti cha usajili namba 32699)

(Imepewa leseni na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kama Mshauri wa Uwekezaji, Mtunza Dhamana na Mshiriki wa Soko la Hatifungani)
(Imeorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) – Alama ya Hisa: “NMB”).



**TAARIFA KWA UMMA
KUHUSU MGAWANYO WA HISA
ZA KAWAIDA ZA BENKI YA NMB**

Benki ya NMB inatoa taarifa kwa umma kuwa mnamo tarehe 24 Julai 2026, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, iliidhinisha mgawanyo wa hisa za Benki ya NMB kwa uwiano wa 1:10, ambapo kila hisa ya kawaida ya Benki ya NMB iliyotolewa na kulipiwa kikamilifu itagawanywa katika hisa kumi (10) za kawaida. Kutokana na hatua hiyo, jumla ya hisa za Benki ya NMB zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) zitaongezeka kutoka hisa 500,000,000 hadi hisa 5,000,000,000. Mgawanyo huu wa hisa unalenga kuongeza unafuu wa bei ya hisa za Benki ya NMB, kuimarisha ukwasi wa hisa za Benki ya NMB sokoni, pamoja na kupanua wigo wa ushiriki, hususani kwa wawekezaji wadogo katika soko la mitaji.

TAREHE ZA MATUKIO MUHIMU

Wanahisa, washiriki wa soko, wawekezaji na umma kwa ujumla wanashauriwa kuzingatia ratiba ya tarehe muhimu zifuatazo kuhusiana na utekelezaji wa mgawanyo wa hisa za Benki ya NMB:

MAELEZO	TAREHE
Tarehe ya tangazo	Jumatatu, 27 Julai 2026
Tarehe ya hisa kuanza kuuzwa pamoja na stahiki ya mgawanyo wa hisa	Jumatatu, 27 Julai 2026
Tarehe ya mwisho hisa kuuzwa pamoja stahiki ya mgawanyo wa hisa	Jumatano, 19 Agosti 2026
Kusimamishwa kwa muda kwa shughuli za uuzaji na ununuzi wa Hisa	Alhamisi, 20 Agosti 2026 mpaka Ijumaa, 21 Agosti 2026
Tarehe ya kufungwa daftari la wanahisa	Ijumaa, 21 Agosti 2026
Maboresho ya daftari la wanahisa	Ijumaa, 21 Agosti 2026 mpaka Jumapili, 23 Agosti 2026
Tarehe ya Utekelezaji rasmi wa mgawanyo wa hisa	Jumatatu, 24 Agosti 2026
Hisa kuanza kuuzwa baada ya mgawanyo	Jumatatu, 24 Agosti 2026

KUSIMAMISHWA KWA MUDA KWA SHUGHULI ZA UZAJI NA UNUNUZI WA HISA

Shughuli za uuzaji na ununuzi wa hisa za Benki ya NMB zitasimamishwa kwa muda kuanzia Jumatano, 19 Agosti 2026 saa 10:00 jioni mara baada ya soko kufungwa. Ili kurahisisha zoezi la mgawanyo wa hisa, oda zote za kuuza na kununua hisa za Benki ya NMB zitazokuwa zimesalia kwenye mfumo wa soko la hisa mara baada ya soko kufungwa zitaifikia ukomo wake mara moja. Wawekezaji ambao oda zao zitakuwa zimefikia ukomo wake wanashauriwa kuziweka tena oda hizo kupitia kwa mawakala wa soko la hisa au mifumo ya kidijitali ya soko mara baada ya soko kufunguliwa siku ya Jumatatu tarehe 24 Agosti 2026.

Aidha, katika kipindi chote cha usimamishaji huo, hakutakuwa na shughuli yoyote ya ununuzi au uuzaji wa hisa za Benki ya NMB itakayoruhusiwa hadi Jumatatu, tarehe 24 Agosti 2026, siku ambayo soko litafunguliwa tena rasmi. Kipindi hiki cha usimamishaji kimetengwa ili kutoa fursa kwa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), CSDR, pamoja na Benki ya NMB, kufanya uhakiki na maboresho ya daftari la wanahisa, ili kuhakikisha kuwa kila hisa moja inayomilikiwa na mwanahisa inagawanywa na kuwa hisa kumi, kwa mujibu wa mgawanyo wa hisa uliopitishwa.

Soko litakapofunguliwa tena Jumatatu, tarehe 24 Agosti 2026, bei ya hisa za Benki ya NMB itafuata taratibu na miongozo ya soko la hisa zinazosimamia mgawanyo wa hisa.

MAELEZO YA ZIADA

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na NMB kupitia barua pepe tuambie@nmbbank.co.tz au simu **0800 002 002**.

Kwa Amri Ya Bodi



Farija Ghikas
Katibu wa Kampuni

TAREHE: 27 Julai 2026

Tangazo hili limetolewa kwa idhini ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa mujibu wa kanuni za Mamlaka za Matangazo, G.N. Namba. 15 ya mwaka 1997.